

SURA YA KWANZA

NAMNA AMANI ILIVYO DUMISHWA NA KUENDELEZWA KATIKA AWAMU YA TANO

Amani ni kitu muhimu katika Taifa lolote duniani bila Amani hakuna kinachoweza kufanyika katika ukanda wa Afrika ya mashariki Tanzania imekuwa nchi ya mfano katika suala zima la Amani.

Kwanini Tanzania inakuwa mfano na kinara katika suala la Amani? Kuna vitu vingi ambavyo Tanzania haifanyi ukitofautisha na mataifa mengine yalivyo tunapo zungumzia Amani hatuwezi kuacha kuwataja waasisi wa Taifa letu,

Mwalimu Julius kambarage Nyerere kwanini tunamtaja Nyerere nikutokana na misingi na miiko aliyo iweka hasa katika suala la Amani.

Ukabira: Rais John pombe Magufuli alifuata nyao za muasisi wa taifa Mwalimu Julius kambarage Nyerere alipinga ukabira alikemea ukabira watanzania sote hatuna ukabira.

Unaweza kuona hata muingiliano wakimahusiano kati ya makabira tulionayo katika nyanja tofauti kiuchumi ndoa hata biashara pia kitu ambacho hakipo katika mataifa jirani yanayo izunguka Tanzania,

Rais Magufuli ameweza kulihubiri mala kwa mala nakuonyesha hali ya kulipnga suala la ukabira lakini hata maendeleo ambayo yamefanywa kwakipindi cha miaka yote ya uwongozi wake hakuyafanya kiukanda wala kikabira ukiachia mbali shutuma zenye mlengwa wa kisiasa.

Shutuma ambazo zilibuliwa na watu wa upinzania hizo huwa ni hoja za kisiasa ila uhalisia maendelo yaliofanywa na Rais John pombe Magufuli hayana mlengwa wa ukabira wala ukanda,

Athari za ukabira ndiyo zinazoweza kuleta uvunjifu wa Amani ndani ya Taifa Rais Magufuli amejitahidi katika eneo zima la Amani kwa vitu vingi vinavyo onekana wazi.

Palipo na watu wengi huwa hapakosi mengi kabla ya uwongozi wa Rais Magufuli kulikuwa na matukio mengi ya ujambazi na unyag'anyi kwa baadhi ya maeneo nchini Raisi Magufuli amezuiya na kupambana na suala hilo upungufu wa wamatukio kama hayo katika uwongozi wake umeonekana,

Matukio ya ujambazi unyag'anyi na ubakaji n.k. huwa yanapo zidi katika jamii yana hatarisha Amani huwa ni kengere ya vita ndogondogo katika jamii kwanini ni vita ndogo? Kunaweza kutokea hali ya malipizi baina ya mtu na mtu unapo fanikiwa kudhibiti mfumko wa matukio kama hayo nikuendelea kuimarisha na kudumisha Amani.

Udini: Niwazi Tanzania haina udini katika mazingira yoyote yale Rais John Pombe Magufuli katika uwongozi wake hakuna uashirio wowote wa udini,

Imeonekana wazi nasi kwa maneno Rais Magufuli katika teuzi zake zote wameteuliwa watu ambao unaweza usijuwe dini zao au madhehebu yao nikutokana na jinsi Tanzania tulivyo zoea kutokuwa na udini.

Udini unahatarisha Amani vita ya kidini ni mbaya kuliko vita yoyote ile watu wanauwana wenyewe kwa wenyewe nchiniyongi zilizo jiingiza katika udini duniani zina pigana kila uchao.

Mzozo wa udini katika jamii ni hatari ashukuriwe Rais Magufuli kwa kuimairsha tunu hii ya Amani akifuata nyendo za Baba wa Taifa hayati Julius Kambage Nyerere.

Kulidhihirisha hilo mwaka 2020 mwezi wa saba nikitua cha tofauti kilicho fanywa na Raisi Magufuli alipo changisha alambee ya ujenzi wa msikiti Dodoma katika eneo la chamwino.

Kwanini ni tukio la tofauti linatufundisha nini hasa kwa viongozi wajao? Kudumisha Amani yetu nakuondokana na dhima mbaya ya udini katika tukio hilo lililofanyika ndani ya kanisa katoriki mapadre walitoa harambee za ujenzi wa msikiti huwo eneo la chamwino.

Hilo nifundisho kubwa kwa viongozi wajao Magufuli kwa kitendo hicho nisawa namtu aliyesema sisi wote ni sawa hakuna mwislamu wala kristu sote tunahitajika kusaidiana nakujiletea maendeleo katika Taifa letu Magufuli ni kiongozi wa mfano wakuigwa Afrika.